# TANGAZO LA KAZI ZA MUDA

*Imewekwa Thursday 28th Mar , 2024*

TANGAZO LA KAZI

KAZI YA MUDA

Wakala wa Ufundi na Umeme Tanzania (TEMESA) ni Taasisi ya Umma iliyoanzishwa kwa Sheria ya Wakala wa Serikali Sura ya 245. Majukumu yake makubwa ni kutoa Huduma za Matengenezo ya Magari na Mitambo, Huduma za Umeme ikiwa ni pamoja na kufanya Matengenezo ya Taa za Barabarani, kufanya Matengenezo ya Majokofu, Viyoyozi na kufanya Matengenezo ya Mifumo ya TEHAMA na Vifaa vya Elektroniki, kutoa Huduma za Vivuko na Huduma za Ushauri.

Meneja wa Kanda ya Mashariki na Kusini, katika kuhakikisha kuwa majukumu ya Wakala yanatekelezwa anatangaza nafasi za kazi za muda kama ifuatavyo:

1. FUNDISANIFU BAHARINI (MARINE) - NAFASI 10

a Sifa za mwombaji:

i. Awe na elimu ya kidato cha sita na kuhitimu kozi ya ufundi ya miaka miwili katika fani ya Baharini (Marine) kutoka chuo kinachotambuliwa na Serikali au

ii. Awe na elimu ya kidato cha nne na kufuzu kozi ya miaka mitatu katika fani ya Baharini (Marine) kutoka chuo kinachotambuliwa na Serikali,au

iii. Awe na elimu ya kidato cha nne na Cheti cha Majaribio ya Ufundi Hatua ya I (Trade Test I) kutoka chuo kinachotambuliwa na Serikali.

iv. Awe na cheti cha mafunzo ya ufundi wa vyombo vya majini (Certificate of Successes Rating Forming Part of an engineering watch course)

v. Awe amefuzu mafunzo ya miezi sita ya uokoaji wa maisha majini na kuogelea.

vi. Awe Raia wa Tanzania.

b Majukumu

i. Kuchunguza, kutambua na kufanya marekebisho ya vivuko/boti.

ii. Kufanya matengenezo ya mashine za kupachika (outboard engines) na mitambo ya mashine za ndani (inboard engines) za vivuko/boti.

iii. Kufanya majaribio ya mitambo ya vivuko/boti baada ya matengenezo.

iv. Kutunza injini, vifaa, vipuli na zana za mitambo ya vivuko/boti

v. Kutunza na kuweka kumbukumbu za kiufundi za vivuko/boti.

vi. Kufanya kazi atakazopangiwa na Mkuu wake wa kazi.

2. NAHODHA WA VIVUKO (FERRY CAPTAIN II) - NAFASI 10

(a) Sifa za mwombaji:

i. Awe na elimu ya kidato cha nne au Cheti cha Juu cha Elimu ya Sekondari (ACSEE)

ii. Cheti cha lazima cha msingi (mandatory Certificate ) kulingana na STCW95 na Ukadiriaji Unaounda Sehemu ya Saa ya Kuongoza (Rating Forming Part of Navigation Watch - RFPAW).

iii. Awe na Shahada ya Kwanza/Stashahada ya Juu/Diploma katika mojawapo ya fani zifuatazo; Sayansi ya Baharini, Uhandisi wa Baharini, Uhandisi wa Mitambo/Kiraia, Uhandisi wa Kielektroniki/Umeme, au nyanja nyingine yoyote inayohusiana ni faida iliyoongezwa

iv. Awe Raia wa Tanzania.

(b) Majukumu

i. Kuendesha kivuko (Pontoon) kutoka sehemu moja hadi nyingine kwa mujibu wa Sheria, Kanuni na Taratibu zinazokubalika kwa ujumla;

ii. Kuondoka, kusafiri, kusimamisha na kuwasiliana kwa usalama kwa mujibu wa Sheria na Kanuni zinazotumika;

iii. Kuzingatia ratiba zilizowekwa za kuondoka na kufika;

iv. Kufuatilia utendakazi wa wafanyakazi wote, kuripoti mwenendo wa kupigiwa mfano na usioridhisha kwa Mkuu wa Kivuko;

v. Kuripoti upungufu au ukiukwaji wowote kwa Kivuko kwa Mkuu wa Kivuko;

na

vi. Kufanya kazi nyingine kama itakavyoagizwa na msimamizi wako.

5. MABAHARIA DARAJA LA II (FERRY DECK ASSISTANT II) – NAFASI 10

(a) Sifa za Mwombaji:

i. Awe na elimu ya kidato cha nne

ii. Awe amemaliza angalau miezi sita ya muda wa Bahari katika huduma za baharini na Vyeti vya Mafunzo ya Lazima (Mandatory courses /refresher in mandatory courses) vinavyotolewa na Taasisi zinazotambuliwa na serikali au Shirika la Kimataifa la Usafiri wa Baharini (IMO)

iii. Kupanga watu na magari kwenye vivuko/boti.

iv. Awe Raia wa Tanzania.

(b) Majukumu

i. Ili kuhakikisha kwamba pontoon ni salama wakati wote kwa uendeshaji;

ii. Kufunga na kufungua kamba za pantoni kwa kutumia waya na kamba wakati pantoni imesimama;

iii. Ili kuhakikisha kwamba staha ya pontoon haina maji na uchafu;

v. Kufuatilia mienendo na mienendo ya abiria wakiwa ndani ya pantoni;

vi. Kusimamia abiria na mizigo yao na kupanga Magari ipasavyo;

i. Kufanya shughuli zingine kama vile rangi, buff na mizani kwa kushirikiana na mafundi;

ii. Kushiriki katika shughuli za uokoaji kila inapohitajika au inapotokea ajali yoyote.

iii. Kufanya kazi nyingine yoyote inayohusiana kama inaweza kuagizwa na msimamizi.

2. FUNDISANIFU VIYOYOZI DARAJA LA II – NAFASI 10

a. Sifa za mwombaji

i. Awe na Elimu ya Kidato cha nne na kuhitimu kozi ya ufundi ya miaka

miwili katika fani ya viyoyozi kutoka chuo kinachotambuliwa na Serikali

au

ii. Awe na Elimu ya Kidato cha Nne na kufuzu kozi ya miaka mitatu katika

fani ya viyoyozi kutoka Chuo kinachotambuliwa na Serikali au

b. Majukumu

i. Kufanya matengenezo ya Viyoyozi, majokofu na Mabarafu (Cold

Rooms).

ii. Kusimika mifumo mipya ya Viyoyozi, majokofu na Mabarafu

iii. Kufanya ukaguzi wa mifumo iliyopo kwenye majengo ya Serikali

inayohusisha Viyoyozi, Majokofu na Mabarafu.

Kufanya kazi atakazopangiwa na Mkuu/Msimamizi

MASHARTI YA JUMLA

i. Mwombaji awe na umri usiozidi miaka 45

ii. Barua za maombi ziambatishwe na nakala za vyeti husika, picha mbili ndogo

(Passport Size) za Mwombaji na taarifa binafsi (Cirriculum Vitae) ya mwombaji

iii. Waombaji watakaokuwa na sifa zinazohitajika ndio watakaoitwa kwenye usali

iv. Barua za maombi zitumwe kwa

MENEJA WA VIVUKO,

KANDA YA MASHARIKI NA KUSINI

TEMESA,

S.L.P. 70704,

DAR ES SALAAM.

N.B.

Tangazo hili limetolewa tarehe 28 MACHI, 2024

Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 15 APRILI, 2024